



## East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 6, Issue 2, 2023

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN  
NATURE &  
SCIENCE  
ORGANIZATION

Original Article

## Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba

Ambrose Ngesa Kang'e<sup>1</sup>\*, Prof. John. M. Kobia, PhD<sup>1</sup> na Dkt. Dorcas M. Musyimi, PhD<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109-60400 Chuka, Kenya.

\* Barua pepe ya mawasiliano: [kangeambrose@gmail.com](mailto:kangeambrose@gmail.com)

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1663>

Tarehe ya Uchapishaji: **IKISIRI**

28 Desemba 2023

**Istilahi Muhimu:**

*Matumizi,  
Usohalisia wa  
Kihistografia,  
Nyimbo za Kisasa,  
Injili.*

Usohalisia ni kipengele muhimu kinachodhihirika katika tungo za kisasa za fasihi. Watunzi wa fasihi ya kisasa hutumia mtindo wa usohalisia kwa namna mbili kuu ambazo ni ujirejelezi wa mtunzi na usohalisia wa kihistografia. Makala haya yamefafanua jinsi usohalisia wa kihistografia ulivyotumika katika nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba. Nyimbo za kisasa za injili za Kikamba zimerejelewa ili kuwakilisha nyimbo za kisasa za injili zilizoimbwa kwa lugha yoyote nchini Kenya. Utanzu wa nyimbo za injili umeteuliwa kwa sababu kutoka miaka ya elfu mbili umedhihirisha mabadiliko si haba ya kuuwasilisha kwa hadhira bali na kuwa utanzu pendwa. Makala haya yametumia mtazamo wa kiusasaleo kuchanganua matini za nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba. Mtazamo wa kiusasaleo hushuku na kupinga mitazamo ya kijadi na kupendekeza mitindo mipya ya kuwasilisha tungo za fasihi ya kisasa. Kutokana na uchanganuzi, iligunduliwa kuwa matumizi ya mtindo wa usohalisia wa kihistografia yalidhihirika kwa namna kadhaa katika nyimbo za injili za kisasa za Kikamba zilizoteuliwa kuchunguzwa. Matumizi ya mtindo wa usohalisia yalidhihirika kupitia utumiaji wa mbinu mbalimbali ambazo zimefafanuliwa na makala haya.

### APA CITATION

Kang'e, A. N., Kobia, J. M. & Musyimi, D. M. (2023). Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), 84-97. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1663>.

### CHICAGO CITATION

Kang'e, Ambrose Ngesa, John. M. Kobia and Dorcas M. Musyimi. 2023. "Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 84-97. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1663>.

### HARVARD CITATION

Kang'e, A. N., Kobia, J. M. & Musyimi, D. M. (2023) "Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 84-97. doi: 10.37284/jammk.6.2.1663.

### IEEE CITATION

A. N. Kang'e, J. M. Kobia, & D. M. Musyimi "Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 84-97, Dec. 2023.

## MLA CITATION

Kang'e, Ambrose Ngesa, John. M. Kobia & Dorcas M. Musyimi. "Matumizi ya Usohalisia wa Kihistografia katika Nyimbo Teule za Kisasa za Injili za Kikamba". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Dec. 2023, pp. 84-97, doi:10.37284/jammk.6.2.1663.

## UTANGULIZI

Fasihi simulizi ni utanzu hai wa fasihi unaowasilishwa kwa ufundi wa kipekee ili kuibua nadharia za kijamii, kisiasa, na kiuchumi (Wamitila, 2008). Aina hii ya fasihi huwa na tanzu nyingi kama vile misemo, methali, vitendawili, maigizo, mighani, ngano, ushairi, na nyimbo (King'ei na Kisovi, 2005). Utanzu wa nyimbo ni kipengele cha utamaduni wa jamii ambacho hubadilika kiwakati ili kuakisi mabadiliko ya historia ya mwanadamu (Omojala, 1987). Utanzu wa nyimbo huwa na aina nyingi za nyimbo ambapo kila aina hurejelea muktada fulani wa kijamii. Miongoni mwa tanzu maarufu za nyimbo hivi leo ni nyimbo za injili ambazo zimeacha taathira kubwa kote ulimwenguni.

Uimbaji wa nyimbo za injili ulianzishwa miaka ya 1800 na wainjilisti Dwight, L. Moody na Ira, D. Sankey (Muathe, 2016). Mtindo ulioanzisha na wainjilisti hao uliotofautiana na uimbaji wa nyimbo tangulizi za sifa (Malone, 1984). Nyimbo walizozianzisha zilikarabatiwa na Wanegro kwa kuunganisha mitindo ya nyimbo za kiroho, za sifa na nyimbo za kidunia. Thomas Dorsey alibadilisha mtindo wa kuimba nyimbo za injili zaidi kwa kuzitunga zikiakisi mtindo wa kidunia uliohusisha mtindo wa kijadi wa nyimbo za sifa na mtindo wa nyimbo za 'jazi'. Mtindo huu ulibadilishwa zaidi na waimbaji Charlse Todley, Lucie Campell and Dr. Isaac Watts ambao walidengua nyimbo za kitamaduni na kuziimba kama za injili (Wise na Stanley, 2002). Hii ni kuonyesha kwamba nyimbo za injili zimekuwa zikibadilisha mitindo ya kuzisimulia, ili kuakisi kila kipindi cha kimaendeleo.

Barani Afrika na hasa nchini Kenya, nyimbo za injili zilianzishwa na Wamishenari miaka ya 1940 zikiwa zimenakiliwa katika vitabu vya nyimbo kama vile *Golden Bells* (Omojola, 1987). Nyimbo hizo zilizingatia mitindo ya nyimbo jadiya za Wanegro (Cockrell, 1987; Chitando, 2000). Baadaye nyimbo hizo zilitafsiriwa kwa lugha za

Kiafrika ambapo mwimbaji David Nzomo alitafsiri baadhi yazo kwa lugha ya Kikamba (Mwendwa, 2020) na huimbwa zikizingatia taratibu za kimapokeo (Akuno, 2007). Uimbaji wa nyimbo za injili kwa lugha za Kiafrika nchini Kenya ulianza miaka ya 1980 (Kidula, 1998). Mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiteknolojia mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000 yaliathiri vipengele muhimu vya kimtindo katika uwasilishaji wa nyimbo za injili kwa hadhira (Ingallas, 2010). Nyimbo za kipindi hiki zimedhihirisha mwondoko kutoka kwa mtindo wa kimapokeo kwa kujaribia mitindo mipya (Nyairo, 2008). Baadhi ya nyimbo za kisasa za injili ziliteuliwa kwa uchanganuzi huu. Madhumuni ya makala haya yalikuwa ni kufafanua matumizi ya usohalisia wa kihistografia katika nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba. Nyimbo za kisasa za injili za Kikamba zilirejelewa ili kuwakilisha nyimbo za kisasa za injili zilizoimbwa kwa lugha yoyote nchini Kenya.

## Mwauo wa Maandishi

Usuli wa dhana ya usasaleo ungali tata hadi wa sasa licha ya baadhi ya wasomi kujaribu kuangazia usuli wake. Kwa mfano, Best na Keller (1991) wanadai kwamba dhana hii ilitumiwa na Arnold Toynbee mwaka wa 1947 katika kitabu chake cha *A Study of History* akionyesha hatua mpya katika historia ya Kimagharibi. Hata hivyo, wasomi hawa wanazua utata zaidi wanaposema kuwa Toynbee (1947) alidahili kuwa dhana hii ilianza kutumiwa 1875. Baadhi ya wasomi hutofautiana kuhusu usuli wa dhana hii. Kwa mfano, Cahoon (1996) hushikilia kuwa dhana hii iliingizwa katika dhana za fasihi za kihakiki miaka ya 1950. Nicol (2009) anadahili kwamba dhana hii iliasisiwa miaka ya 1940 katika usanifu wa majengo kupinga mawazo ya kimapokeo. Hata hivyo, wanakubaliana kwamba ni dhana iliyotumiwa kurejelea sanaa zilipinga masuala ya kitamaduni kama vile matini ya kifasihi,

mawasiliano, sanaa za maonyesho na usanifu wa majengo baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Hivyo, inahalisi kusema kwamba dhana hii ilinawiri na kutumika katika uwanja wa fasihi kufikia miaka ya 1960 ili kupinga mtazamo wa kimapokeo.

Taylor na Winquist (2002) wanadahili kwamba dhana ya usasaleo iliibuka kupinga mawazo ya kijadi kuhusu umoja, upendeleo, epistemolojia, ujumi, maadili, historia na siasa. Malpas (2005) na Nicol (2009) wanaona usasaleo kuwa ni mabadiliko ya kisanaa yanayodhihirisha hatua ya juu zaidi ya utamaduni wa kikapitalisti unaohusishwa na mitindo na kuwasilisha sanaa. Harvey (1989) anakiri kwamba usasaleo ni dhana tata na hakuna mtu ajuaye maana yake hasa ila inakisiwa tu kuwa ni mwondoko kutoka kwa usasa. Anaungwa mkono na Hutcheon (1988) akisema kuwa usasaleo ni mwondoko hasa kutoka kwa usasa. Kwa mujibu wa Hicks (2004), wakareketwa wa usasaleo hushuku urazini, ukweli na uhalisia wakidai kwamba ni simulizi kuu zisizo thabiti na razini kama inavyofikiriwa. Aidha, anazona simulizi hizi zikiwa ni za kimagaribi, zenye kukandamiza na kuvuruga jamii na hivyo zafaa zitupiliwe mbali na badala yake simulizi ndogondogo zitumiwe kusambaza maarifa.

## TAFITI ZILIZOFANYWA

Wasomi wamechunguza kazi za fasihi kwa mtazamo wa kiasasaleo na kugundua kwamba watunzi wa kimajaribio hutumia mitindo mbalimbali kuwasilisha kazi zao. Kramer (1996) alidhihirisha kauli hii kwa kuchunguza mitindo ya kimajaribio katika nyimbo za Beethovens ambazo ni *String Quarter*, *Ives Putmans Camp* na Mahler *Seventh Symphony*. Msomi huyu alitambua kuwa mitindo ya mwingiliano matini, unukuzi na brikolojia ilitumika katika nyimbo hizo. Utafiti wake ulichanganua mitindo inayoshabikiwa na wakareketwa wa mtazamo wa kiasasaleo na hivyo mawazo ya msomi huyu yalitoa mwelekeo wa kuhakiki nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba.

Ritgerotil (2006) alichunguza matumizi ya mitindo ya kiasasaleo katika filamu teule ya *The*

*Simpsons*. Mtafiti huyu aligundua kuwa katika filamu hii mitindo ya kiasasaleo kama vile mwingilianomatini, usohalisia, simulizi ndogondogo na uundaji wa simulizi kwa njia ya kubeza ilitumiwa kuendeleza usimulizi wa filamu hiyo. Ugunduzi sawa na huu ulidhihirishwa na Gloag (2012) alipochunguza nyimbo za John Cage, Dj Spooky, George Rochberg na John Zorn na kutambua kwamba zimetumia simulizi ndogondogo za visa visivyooana katika nyimbo husika. Mitindo waliyoitambua huendana na kazi za fasihi ya kimajaribio na hivyo matokeo ya tafiti zao yalitumiwa kuchanganua data ya nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba ili kufanua matumizi ya usohalisia wa kihistografia.

Kimugung (2015) alichunguza matumizi ya mitindo mamboleo katika nyimbo teule za jamii ya Kikalenjin za karne ya ishirini na moja. Aliongozwa na Nadharia ya Ubaadausasa ambayo hupinga simulizi kuu. Msomi huyu alitambua kwamba baadhi ya mitindo mamboleo iliyotumika katika nyimbo alizozichunguza ni pamoja na simulizi ndogondogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, uigaji wa vipande vya simulizi na mwingilianomatini. Aidha, Tenna (2019) alichunguza matumizi ya baadhi ya vipengele vya kimajaribio akirejelea riwaya teule za waandishi wa Ethiopia walio mataifa ya nje na kugundua kuweco kwa mwingilianomatini miongoni mwa mitindo mingineo. Mawazo ya wasomi hawa yalitoa uelewa wa mtazamo ya nadharia za ubaadausasa na kisha yakashirikishwa katika uundaji wa vigezo vilivyotumiwa kuchanganua data ya nyimbo teule za injili za kisasa za Kikamba.

## NADHARIA YA UTAFITI

Makala haya yalitumia vigezo vya kiasasaleo vilivyoundwa kutoka kwa Nadharia za Baadausasa kama inavyopendekezwa na Lyotard (1984), McHale (1987), Hutcheon (1988) Lewis (2001) na Bary (2002). Nadharia ya Baadausasa hushuku na kupinga taratibu zinazosisitizwa na Wanausasa kuhusu sanaa, fasihi na utamaduni. Vigezo vilivyotumika kuchanganua data ni pamoja na:

- Matumizi ya usohalisia katika tungo za kiuusasaleo. Kigezo hiki kilitumiwa kufafanua matumizi ya usohalisia wa kihistografia katika nyimbo teule za injili za kisasa za Kikamba ili kutilia shaka taratibu za kimapokeo.
- Matumizi ya vipande vya simulizi. Kigezo hiki kilitumiwa kuchanganua vipengele vilivyozoeleka kama vile ploti, maudhui, mandhari na wahusika na ambavyo katika tungo za kimajaribio hupinduliwa katika uwasilishaji wa nyimbo husika.

### Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanywa maktabani kulikopatikana data ya sekondari na data ya kimsingi. Mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi maksudi wa kinasibu kuteua sampuli ya nyimbo kumi kutoka kwa jumuiya ya nyimbo mia moja zilizokusanywa kutoka kwa waimbaji kumi walioimba zaidi ya nyimbo kumi za kisasa za injili za Kikamba. Kiwango hiki cha sampuli kilizingatia mapendekezo ya Mugenda na Mugenda (2003) kwamba asilimia kumi (10%) ya jumuiya lengwa inaweza kuteuliwa kuwa sampuli ya utafiti. Nyimbo zilizoteuliwa zilidhihirisha utumiaji wa usohalisia wa kihistoria kwa njia moja au nyingine. Mbinu ya kithamano ilitumiwa kwa uchanganuzi huu. Utafiti ulitumia orodha kaguzi kama kifaa cha kukusanya na kuchanganua data. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulifanywa kwa njia ya maandishi na mijadala ya maelezo ya moja kwa moja na kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Usikilizaji wa makini wa nyimbo husika ulifanywa kwa mara kadhaa, kuzinakili kwa Kikamba na kisha kuzitafsiri kwa Kiswahili. Vifungu vilivyodhihirisha matumizi ya usohalisia wa kihistografia vilipangwa kulingana na matumizi husika na kujadiliwa kwa njia ya mijadala ya maelezo vikiwa katika lugha asilia. Nyimbo za injili za Kikamba za kisasa zilizoteuliwa ziwe kiwakilishi cha nyimbo zozote zile za kisasa za injili.

### Uchanganuzi wa Data

Matumizi ya usohalisia wa kihistografia yalichanganuliwa na kufafanuliwa kwa kuangazia

nyimbo teule za injili za kisasa za Kikamba. Nyimbo zilizoteuliwa kwa uchanganuzi ni kama vile *Kunika Munuka* (Funika Kinywa) na *Umo Waku* (Usuli Wako) zilizozimbwa na Wilberforce Musyoka; *Thina Waku* (Shida Yako), *Mundu wa Kana* (Mtu wa Nne) na *Kala Kateoneka* (Yule Asiyeonekana) zilizozimbwa na Abed Musyoki; *Molitikai* (Modekai) wa Juma Justus; *Ningwina* (Ninaimba) na *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) za Scholar Mumo; *Kalonde* (Kondoo) wa Barnabas Matundu na *Utao* (Wosia) wa Purity Kateiko. Makala yalidhihirisha kuwoko kwa vipengele kadhaa vya kiusohalisia wa kihistografia ambavyo vimetumika kufafanua matumizi ya usohalisia katika nyimbo teule za kisasa za injili za Kikamba zilizochanganuliwa.

### USOHALISIA WA KIHISTOGRAFIA

Watunzi wa nyimbo za kisasa za injili zilizoteuliwa wametilia shaka baadhi ya simulizi kuu kama vile dini, uongozi, historia, simulizi kuu za sayansi, pamoja na taasisi nyinginezo za kijamii. Watunzi wa nyimbo hizi wamefanya juhudi kuhakiki simulizi kuu kwa kuzingatia mitazamo tofauti na hivyo kuangazia umatini, mtazamo wa kijadi pamoja na hali gandamizi ya simulizi kuu. Usohalisia wa kihistografia umetumiwa katika nyimbo teule za kisasa za injili kwa nia ya:

### Ukosoaji wa Simulizi za Kihistoria

Tungo za kiuusasaleo huchochewa ili kuzua mabadiliko dhidi ya simulizi za kihistoria. Kuhusu kauli hii, D'haen Theo (1995) ni mwondoko kutoka simulizi kuu unaohusisha utungaji wa kazi za fasihi kwa mtindo wa utohalisia wa kihistografia. Waimbaji wa nyimbo za kisasa za injili zilizochanganuliwa wameonyesha mtazamo unaotilia shaka simulizi za kihistoria ambazo hushikiliwa na jamii ya Wakamba. Kwa mfano, katika wimbo *Thina Waku* (Shida Yako) Abed Musyoki amekosoa mila na desturi za wanajamii kuamini zaidi kinga inayotokana na vifaa vya kiganga. Mwimbaji huyu amefanya hivi kwa kutumia maswali ya balagha. Tazama *Kielelezo 1*.

**Kielelezo 1**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Muu ni waki, mbingiloni sya muthui?</i>	Majivu ni ya nini malangoni mwa tajiri?
<i>Kitoo ni kyaki, mbingiloni sya muthui?</i>	Vumbi ni ya nini malangoni mwa tajiri?
<i>Itani iithiniw'a ki, na itina makosa?</i>	Matambara yasumbuliwa kwa nini, na hayana makosa?

Kulingana na *Kielelezo 1*, mwimbaji ametilia shaka imani iliyokita mizizi katika jamii ya Wakamba kwamba vitu vya kishirikina kama vile majivu na matabara vinaweza kuwekwa malangoni mwa watu kuwazuia wasipatwe na madhara. Vitu vya namna hutumiwa katika jamii ya mwimbaji kuendeleza imani ya kishirikina. Abed Musyoki ametumia mhusika Tajiri kuonyesha kuwa matajiri ndio hasa hushiriki kwa mambo ya kiganga na hivyo anakosoa imani kwamba wanajamii wa kiwango cha chini ndio huwa washirikina kwa kumsawiri tajiri akiwa ameweka vitu hivi malangoni pake ili view kinga kwake na kwa mali yake.

Ukosoaji wa simulizi za kitamaduni ulidhihirika katika wimbo *Kalondo* (Kondoo) ulioimbwa na Barnabas Matundu. Hii ni kulingana na mawazo ya Hutcheon (1988) yanayopinga na kushuku historia moja kama chanzo cha ukweli na kupendekeza uundaji wa historia mbadala. Kulingana na mila na desturi za Wakamba, iwapo kumetokea shida katika familia na wazazi wakose kutambua kiini chake huenda kufanyiwa uganguzi. Mwimbaji amesimulia jinsi mama na baba yake walivyoenda kwa waganga wakitafuta uzima wa mwili wake lakini bila mafanikio. Tazama *Kielelezo 2*.

**Kielelezo 2**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Mwaitu waendie kwa awe</i>	Mama ulienda kwa waganga
<i>Nau waendie kwa awe</i>	Baba ulienda kwa waganga
<i>Maimantha thayu wakwa x2</i>	Wakitafuta maisha yangu x2
<i>Nau watata kuausya,</i>	Baba ukajaribu ugaguzi
<i>Watata kuminza ngoma</i>	Ukajaribu kutingiza hirizi
<i>Indi iandethya</i>	Lakini hazikusaidia
<i>Mami sisya Kaivali</i>	Mama tazama Kalivari.

Kwa mujibu wa *Kielelezo 2*, mwimbaji aeonyesha jinsi alivyogangwa na kuganguliwa na mganga pasipo kusaidika licha ya mganga kutumia hirizi zake zote. Kupitia kisa hiki, Abed Musyoki ametilia shaka mwelekeo wa utamaduni wa Wakamba unaosisitiza kwamba 'ng'ondu' (kifaa fulani cha kiuganga) kina suluhisho kwa shida za wanajamii. Barnabas Matundu ameshambulia dhana hii akionyesha kuwa ni dhana potovu iliyo akilini mwa wanajamii na ambayo haina uhalisia. Mwimbaji ameshambulia na kutilia shaka mwelekeo wa jamii ya Wakamba wa kuweka imani kwenye historia iliyopitwa na wakati na ambayo haitoi suluhu kwa shida za wanajamii. Amesisitiza hili kwa kusimulia akisema "Nau watata kuausya, watata kuminza ngoma indi iandethya" (Baba ukajaribu kuaguliwa, kwa kutikisa hirizi lakini hazikusaidia). Barnabas

Matundu ameipendekezea jamii yake na hasa wazazi wamtazame Yesu mwana kondoo wa Mungu aliyetolewa na kusulubishwa msalabani Kalivari kwa ajili ya kupata suluhisho ya shida zao.

Upingaji wa simulizi za kitamaduni (kihistoria) ulitambuliwa katika wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) ulioimbwa na Scholar Mumo. Upingaji huu wa simulizi kuu unaendana na mawazo ya McHale (1987) yanayoshuku na kupinga historia kama chanzo pekee cha ukweli. Scholar Mumo ameshambulia mwelekeo wa kitamaduni unazosisitiza utumiaji wa *mithea* (dawa za kiganga) na *ithitu* (hirizi) kama njia ya kupata kinga na suluhu ya shida za wanajamii. Tazama *Kielelezo 3*.



**Kielelezo 3**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Mbona yila muthi kwa andu awe mukakue, Mithea na ithitu muyiutala ngalama, Muinengane mbesa mbingi, makili mamilioni, Indi nyumbani ya Ngai muyete kivuthya.</i>	Mbona mkienda kwa waganga mkibeba Dawa na hirizi, hamhesabu gharama Mkipeana pesa nyingi maelfu mamilioni 39. Ila nyumbani mwa Mungu mwaleta dharau

Kwa mujibu wa *Kielelezo 3*, mwimbaji amepinga na kutilia shaka desturi ya ya kitamaduni inayosisitiza utumiaji wa *mithea* (dawa za kiganga) na *ithitu* (hirizi) kwa ajili ya matibabu na usalama wa jamii. Aidha, amekosoa desturi ya wanajamii ya kupeleka mamilioni ya pesa kwa waganga ili wasaidike. Scholar Mumo amewasuta wanajamii wa namna hii kwa kuwaambia hawahesabu gharama lakini wakienda kumwabudu Mungu makanisani hufanya madharau. Hivyo, Mumo, sawa na Matundu na Musyoki, ameshambulia simulizi za kitamaduni ambazo zimekuwa zikipokezanwa na wanajamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuonyesha kwamba zimepitwa na wakati na badala yake wamtumainie Mungu kwa utatuzi wa shida zao.

**Kutulia Shaka Uwezo wa Historia wa Kusimulia Uhalisia Kamili**

Mtindo wa usohalisia wa kihistografia ulitumiwa na baadhi ya waimbaji kuonyesha mtazamo wa

**Kielelezo 4**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Mbona vau tene a susu na umau, Mainaa kilumi, masungaa na kukwatika.. Onenyu umunthi, yila mukwina ndanzi,</i>	Mbona hapo zamani akina nyanya na mababu Waliimba <i>kilumi</i> , walicheza hadi kupangawa Hata ninyi leo, wakati mnaimba densi

*Kielelezo 4* kinadhihirisha kuwa mwimbaji wa wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) umesimulia uhalisia kuhusu uimbaji na uchezaji wa *kilumi* ambao hauwezi kuthibitishwa. Hii ni kwa sababu usimulizi wa huu umetegemea au kurejelea simulizi ambazo tayari zimekuwako na ambazo zimekuwa zikitambwa kwa njia ya mdomo. Hivyo, uhalisia unaosimuliwa katika wimbo huu hausadikiki kwa sababu usuli wake ni simulizi za kitamaduni ambazo zilisimuliwa kwa njia ya mdomo na huenda zilibadilika kiwakati na hivyo kukosa uhalisia kamili.

historia kama bunilizi iliyotumia matini yaliyoteuliwa pasipo ushahidi wa kutosha. Mtazamo huu umeendelezwa na Scholar Mumo katika usimulizi wa wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu). Uhakiki wa usimulizi huu ulionyesha kwamba matini ya kihistoria yaliyotumiwa katika utunzi wa wimbo huu hayarejelei uhalisia wa jinsi mambo yalivyokuwa yakifanywa. Aidha, mwimbaji alitumia matini ya kihistoria ambayo aliweza kuyakumbuka tu na ambayo hayasawiri uhalisia kamili. Hii ni kulingana na mawazo ya kiusasaleo yanayoendelezwa na Hutcheon (1988) kwamba chanzo cha tungo za kihistoria na bunilizi huwa ni uhalisia lakini si uhalisia kamili lakini ni umatini na miundo ya usimulizi. Yanayosimuliwa na Scholar Mumo hayadhihirishi uhalisia kamili bali yanadhihirisha uhalisia wa wimbo alioubuni tu. Tazama *Kielelezo 4*.

Watunzi wa tungo za usohalisia wa kihistografia hutulia shaka uwezo wa historia wa kusimulia uhalisia kamili. Kuhusu hili, Hutcheon (1988) anaeleza kwamba mawazo ya usohalisia wa kihistografia hupinga historia moja kama chanzo cha ukweli na kupendekeza kuwepo na nafasi ya kutunga upya simulizi zao wakipinga simulizi za historia. Wimbo wa *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) ulioimbwa na Scholar Mumo ulidhihirisha ukweli wa mawazo haya. Usimuliaji wa wimbo huu, umerejelea maandiko ya kihistoria yaliyo katika Biblia Kitabu cha Isaya 14:11-12 na ambayo mtunzi na ambayo anawataka walengwa wake wayasome na kuyafasiri vizuri ili wapate

kuelewa ukweli asilia wa ibada ya uimbaji.

Tazama *Kielelezo 5*.

### Kielelezo 5

Kamba	(Tafsiri)
<i>Mwitinda muyasya uthaithi ni mwalyule, Somai mbivilia na muimyalu nesa, Satani ai mwalimu wa uthaithi ituni, Atanamba kwika nai na kwikwa kuu nthi.</i>	Mwashinda mkisema ibada imegeuzwa, Someni Bibilia na kuifasiri vizuri. Shetani alikuwa mwalimu wa sifa mbinguni Kabla kufanya dhambi na kutupwa duniani.

Kulingana usimulizi wa kielelezo cha 5, mwimbaji anaonyesha kuwa Shetani alikuwa mwalimu wa ibada huko mbinguni kabla ya kufanya dhambi na kutupwa duniani. Usimulizi wa tukio la Shetani kuwa kiongozi wa ibada unamfanya msikilizaji atilie shaka ukweli wa historia ya kibiblia. Hii ni kwa sababu maandishi

ya kihistoria aliyoyarejelea ni tofauti na maelezo ya usimulizi wa wa wimbo husika. Maandishi ya kihistoria aliyoyarejelea yamesimulia kuhusu kuanguka kwa Shetani kutoka mahali pake pa sifa. Tazama *Kielelezo 6* kutoka Biblia Takatifu Kitabu cha Isaya 14:11-12.

### Kielelezo 6

Kamba	(Tafsiri)
<i>Winenevyo waku nutheew'e Seoli, vamwe na mawasya ma tunanda twaku: walanilw'e kiinyu, na iinyu niukwivw'ika. Kai wi muvaluku kuma ituni we ndata ya muthenya, mwana wa kioko! Utemetwe ukavikw'a nthi, we ula wavalukilye i mbai nthi!"</i>	Fahari yako imeshushwa hata kuzimu, pamoja na sauti ya vinada vyako; Umetandaziwa funza chini yako, na vidudu vinakufunika. Kumbe umeanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa mpaka chini, Ewe uliyewaangusha mataifa chini

Kwa kurejelea *Kielelezo 6*, inabainika kuwa mwimbaji wa wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) amejiundia historia mbadala kusimulia fasiri ya ujumbe ulioendelezwa katika kifungu cha Biblia kilichorejelewa kwenye kielelezo cha 6. Hii ni kulingana na Hutcheon (1988) anaeleza kwamba mawazo ya usohalisia wa kihistografia hupinga historia moja kama chanzo cha ukweli na kupendekeza kuwepo na nafasi ya kutunga upya simulizi zao wakipinga simulizi za kihistoria zenye kuaminika kuwa ndio pekee hutoa ukweli. Aidha, kielelezo cha 6 ni rekodi ya kihistoria isiyomsawiri Shetani akiwa mwalimu wa ibada mbinguni bali imesimulia kuanguka kwake kutoka mbinguni kwa sababu ya fahari. Hivyo, wimbo huu hauakisi uhalisia kamili. Ikiwa mwimbaji ametumia kifungu hiki cha historia kuelezea uhalisia wa jinsi hali ilivyokuwa awali, basi historia haiwezi kuwasilisha kila kitu kwa ukamilifu wake. Kwa hivyo, wimbo umesimuliwa kwa namna inayomfanya msikilizaji afasiri

uhalisia kwa namna mbalimbali na hivyo kumwezesha kupata uwingi wa maana.

### Kukosoa Mtazamo wa Uongozi kwa Misingi ya Kijadi

Watunzi wa baadhi ya nyimbo teule za kisasa za injili wamekosoa historia inayosisitiza uongozi kwa misingi ya umri. Kwa mfano, Wimbo *Kala Kateoneka* (Yule Asiyeonekana) ulioimbwa na Abed Musyoki umekosoa historia inayoshabikia uongozi kwa misingi ya mtoto wa kwanza wa kiume. Hii ni kwa kuzingatia mawazo ya McHale (1987) kwamba utumiaji wa historia mbadala ili kupinga ujadi katika tungo za kisasa. Ujadi unaoshikiliwa na jamii ya Wakamba ni kwamba uongozi na hasa wa kifamilia humwendea mtoto wa kwanza wa kiume. Abed Musyoki amekosoa mtazamo huu wa kitamaduni katika wimbo *Kala Kateoneka* (Yule Asiyeonekana) kwa kumsawiri kifunga mimba akitawazwa kuwa mfalme wa taifa la Israeli. Tazama *Kielelezo 7*.

**Kielelezo 7**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Samueli avika musyi wa Yese, Yese aumilya ngumbau mbee wake. Samueli esisya Eliavu Akoona kiungamo, Samueli esisya Eliavu Ikithathi ya Yese Ngumbau syonthe syavita, Mauta malea kwitika Anga ndisiasya ta mundu, Nye Ngai nisiasya ngoo. Ndisiasya, umbe kana mbaisepsi.</i>	Samweli akafika kwa Yese Yese akatoa mashujaa mbele yake Samweli anaangalia Eliavu Akaona alivyo kimsimamo Samweli anaangalia Eliavu Kifungua mimba kwa Yese Mashujaa wote wakapita, Mafuta yakakataa kumwagika Eti siangalii kimwanadamu Mimi Mungu huangalia moyo Siangalii umbo ama misuli.

*Kielelezo 7* kinasimulia kuhusu Samweli akifika nyumbani kwa Yese baada ya kutumwa na Mungu aende kumtawaza mfalme wa Israeli. Samweli anapofika kwa Yese anaanza kutumia misingi ya kimwanadamu kama vile umbo na kuzaliwa ili kumpata mfalme husika. Hata hivyo, walioonekana kuwa ndio walistahili walipita mbele ya Samweli lakini mafuta yakakataa kumwagika hadi pale Daudi ambaye hakuwa nyumbani alipoletwa. Kupitia kisa cha kutawaza kwa Daudi kuwa mfalme wa Israeli, mtunzi ameonyesha kwamba historia ni ya watu wenye nguvu au watambulikanao katika jamii. Hivyo, kuteuliwa na kutawaza kwa Daudi kuwa mfalme wa Israeli kunaandikisha historia mpya kuhusu dhana uongozi katika taifa la Israeli. Uteuzi na kutawazwa kwa Daudi kuwa mfalme ni kinyume na matarajio ya babake mzazi ambaye mwanzoni aliwatoa wana aliowaona kuwa wanafaa kuongoza. Kupitia kisa hiki mwimbaji amekosoa utoaji wa uongozi kwa misingi ya nani ni nani katika jamii.

Mwelekeo wa Yese umetokana na mtazamo wa kihistoria ulioshikiliwa na Wayahudi kwamba uongozi wa familia ulimwendea mtoto wa kwanza wa kiume. Hii ndio sababu Yese alianza kuwatoa wanawe wakifuatana kulingana na jinsi walivyojaliwa. Mtunzi ameonyesha kukataliwa kwa historia ya kiubabe na historia ya nani ni nani katika jamii pale wana wa Yese aliowahesabu kuwa ndio walifaa kuongoza Israeli walipopita wote lakini mafuta ‘yakakataa’ kumwagika. Kuhusu mtazamo huu Hutcheon (1988) anaeleza kwamba tungo za kiusohalisia wa kihistografia husawiri mkinzano kati ya maandishi ya kihistoria, hudharau kanuni za kijadi na kuingiza uhistoria na uhalisiajabu. Mafuta yalikataa kumwagika ili kudhihaki uteuzi wa kibinadamu kwa misingi ya kihistoria na hivyo kupinga taratibu zilizowekewa taasisi za kijamii na wajadi. Aidha, kisa cha kutawazwa kwa Daudi kimeonyesha kwamba uteuzi wa Mungu ni tofauti na wa mwanadamu. Hivyo, yule asiyeonekana kuwa afaa machoni mwa watu huenda akawa ndiye afaaye zaidi machoni mwa Mungu kufanya kazi yake. Tazama *Kielelezo 8*.

**Kielelezo 8**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Ninisi ndwonekaa, angi mayoneka. Ninisi ndutalawa, angi maitalwa. Ndaviti ndooneka, angi mayoneka. Ndaviti ndatalawa, angi maitalwa</i>	Najua huonekani, wengine wakionekana Najua huhesabiwi, wengine wakihesabiwa Daudi hahesabiwi, wengine wakihesabiwa Daudi haonekani, wengine wakionekana

Kulingana na *Kielelezo 8*, mwimbaji amekosoa dhana ya kijadi kuhusu kiongozi kwa kupinga wazo la kuteua mfalme kwa misingi ya historia ya kuzaliwa na kuonyesha kwamba uteuzi wa namna

hii haufai. Aidha, ameonyesha kuwa mtazamo wa kijadi unafaa uchunguzwe upya na kisha ubadilishwe. Mtazamo ambao mwishowe umetumiwa kumtawaza kifunga mimba



unaendana na mawazo ya McHale (1987) na Hutcheon (1988) kwamba mtindo wa usohalisia wa kihistografiauingiza simulizi za pembeni ambazo hazikupewa thamani kwenye muktadha ili kupuuza simulizi kuu kuhusu historia na uongozi.

### Uchanganyaji wa Uhalisia na Fantasia

Uchanganyaji wa hali halisi na fantasia ni mtindo wa usohalisia wa kihistografia. Baadhi ya nyimbo za kisasa za injili zilizoteuliwa zimedhihirisha matumizi ya mtindo huu. Uchanganyaji wa uhalisia na fantasia ni mtindo ambao hutumiwa na mtunzi kuonyesha kuwa historia hubuniwa na

wanajamii na kwamba ni hadithi zilizopokezwa kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo. Kwa mfano, Barnabas Matundu ametumia uchanganyaji wa uhalisia na fantasia kusimulia maudhui ya wimbo *Kalonde*. (Kondoo). Katika wimbo huu, Barnabas Matundu amesimulia uhalisia wa utafunaji miraa na uvutaji bangi ambao umekidhiri katika jamii ya Wakamba ya sasa. Aidha, kwa namna ya kifantasia ameweka wazi madhara ya utumiaji wa bangi. Amefanya hivi kwa kutumia mhusika Mama na mhusika Baba na kuwasawiri wakiwa wamevuta bangi hadi wakawa wanazungumza peke yao wakitembea barabarani. Tazama *Kielelezo 9*.

### Kielelezo 9

Kamba	(Tafsiri)
<i>Nikwone nziani,</i>	Nilikuona njiani
<i>Mwaitu uyikya moko.</i>	Mama ukitupa mikono
<i>Nikwone nziani,</i>	Nilikuona njiani,
<i>Nau uineena weka.</i>	Baba ukizungumza pekee
<i>Wineenw'a mana niki?</i>	Wazungumza ovyo kwa nini?
<i>Wineena wi weka niki?</i>	Wasema ukiwa pekee kwa nini?
<i>Wikya moko maki?</i>	Watupa mikono ya nini?
<i>Vangi winywa waki?</i>	Bangi wavuta kwa nini?

Kwa kurejelea *Kielelezo 9*, mwimbaji amefikiria madhara ya uvutaji bangi na kubuni matini yenye kuakisi madhara haya. Ili kuchanganya uhalisia na fantasia, mwimbaji amebuni wahusika Mama na Baba wakidhihirisha madhara ya utumiaji wa dawa za kulevya. Barnabas Matundu hasimulii uhalisia kamili wa tukio hili ila amefikiri na kuunda matini mbadala ya kusimulia lengo la wimbo wake. Wahusika anaowataja kama aliwaona njiani ni wahusika wa kifantasia tu na wala si wahusika wa kihalisia. Hivyo, uhalisia wanaouwakilisha ni uhalisia wa ulimwengu wa wimbo tu na wala si uhalisia wa ulimwengu halisi. Hata hivyo, amechanganya uhalisia na fantasia ili kusawiri hali halisi ya jamii anayoilenga. Matumizi ya kuchanganya uhalisia na fantasia yanaendana na mawazo ya Hutcheon (1988) yanayosisitiza kwamba uchanganyaji wa uhalisia na fantasia hupinga ujumuishaji wa ukweli na kupendekeza kuweco kwa kweli nyingi.

Suala la kuwepo kwa waganga wanaoagulia wanajamii shida zao ni la kihalisia katika jamii ya mtunzi. Hata hivyo, mtunzi amechanganya uhalisia na uwongo alioubuni kutokana na mafikra na ufahamu wake wa simulizi za kihistoria za jamii yake ili kusawiri ushirikina. Kwa kufanya hivi, mwimbaji amebuni historia mbadala kusimulia hali halisi ya jamii yake. Hii ni kulingana na mawazo ya Hutcheon (1988) kwamba kamwe hakuna ukweli mmoja wa kihistoria na si eti kwamba hakuna uongo lakini kuna kweli za wengine. Hao wengine ni wale ambao hawakuangaziwa na historia ambayo hupendelea walio na nguvu na vyeo. Mwimbaji amedhihirisha ufahamu wa jinsi uganga na uganguzi huendelezwa katika jamii yake na hivyo kwa njia isiyo wazi, kutoa njia mbadala ya kupata suluhu ya shida maishani. Tazama *kielelezo 10*.

**Kielelezo 10**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Mwaitu waendie kwa awe, Nau waendie kwa awe Maimantha thayu wakwa x2 Nau watata kausya, Watata kuminza ngoma Indi iandethya</i>	Mama ulianda kwa waganga Baba ulianda kwa waganga Wakitafuta maisha yangu x2 Baba ukajaribu ugaguzi Ukajaribu kutumia hirizi Lakini hazikunisaidia

*Kielelezo 10* kimweka wazi kwamba msimulizi amesimulia ukweli na wakati ule ule amesimulia uwongo kwa kubuni matini kutokana na ufahamu wake wa historia ya jamii yake ili kuendeleza dhamira na maudhui ya wimbo wake. Hii ni kumaanisha kwamba amesimulia nusu ukweli na nusu uwongo na hivyo kumsukuma msikilizaji wake atilie shaka uhalisia wa wimbo wake.

**Kukuza Mvutano baina ya Kizazi cha Kisasa na Kizazi cha Kale kuhusu Uhalisia**

Watunzi wa baadhi ya nyimbo zilizochanganuliwa walitumia mtindo wa usohalisia wa kihistografia kukuza mgogoro baina ya kizazi cha kijadi na kizazi cha kisasa kuhusu uhalisia. Uhalisia wa simulizi katika nyimbo za

kisasa za injili hutegemea umesimuliwa na kundi lipi - la kijadi au la kisasa. Kwa mfano, katika wimbo *Ningwina* (Ninaimba) usimulizi kuhusu ukweli wa uimbaji wa nyimbo za injili ni kamba ya mvutano baina ya wajadi na kizazi cha kisasa. Scholar Mumo katika wimbo *Ningwina* (Naimba) ameukuza mvutano huu kutoka mwanzo hadi mwisho wa usimulizi wake. Kupitia mvutano unaoakuzwa, mwimbaji amewafanya wasikilizaji watilie shaka uhalisia ulio kwenye wimbo husika. Wazee na akina mama wanasema uimbaji wa kizazi kipya ni densi na wala si wa nyimbo za injili huku nao waimbaji wa kisasa wakiuona wenye kufaa zaidi kumsifu na kumtukuza Mungu wao. Tazama *Kielelezo 11*.

**Kielelezo 11**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Mwaisye ni ndanzi wathi usu ti wa gospel. Tene wathi wa Ngai ko winawa ata? Na vaandikitwe va mbiviliani na muitwonavya?</i>	Mlisema ni densi wimbo huo si wa injili. Kwani wimbo wa Mungu huimbwa vipi? Na imeandikwa wapi katika Bibilia na hamtuonyeshi?

*Kielelezo 11* kinaonyesha kwamba hakuna kundi lililo na ukweli wa uimbaji wa nyimbo za injili ulio mwafaka. Hivyo, kutokuwa na uhakika wa jinsi nyimbo za injili zinavyostahili kuimbwa kumemfanya msikilizaji awe na shaka ni mwelekeo upi au fuata. Aidha, hali hii imetatanisha msikilizaji na kumfanya aione historia yenye kusimuliwa kama lililobuniwa tu na makundi yanayolumbana.

Mwimbaji wa wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) amekuza mvutano ambao umetilia shaka taratibu za kijadi za kuhusu uimbaji wa nyimbo za injili. Aidha, Scholar Mumo ametambua juhudi za wapinzani wake za kuweka taratibu ambazo kulingana nao zinafaa kumwabudu Mungu kupitia uimbaji wa nyimbo za injili. Hata hivyo, anawasiwasi kwamba hizi ni taratibu bandia tu na kamwe hazina uasililia. Tazama *Kielelezo 12*.

**Kielelezo 12**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Wikite vitii kana Ngai ndakathaithwe Kana Ngai ndakataiwe indi tumai Metho mwone tuina na kusunga.</i>	Umetia bidii ili Mungu asiabudiwe Ili mungu asisifiwe, lakini tumeni Macho muone tukiimba na kucheza

*Kielelezo 12* kimesimulia juhudi za wapinzani wa uimbaji wa kisasa wa nyimbo za injili. Wapinzani ambao wamerejelewa ni wajadi ambao wamezidi kushikilia kanuni za kizamani za kuimba nyimbo za injili. Scholar Mumo ametambua juhudi za wavyele za kupinga Mungu asiabudiwe kwa nyimbo za mitindo ya kisasa. Ili kusisitiza

pingamizi zao, wajadi wameshikilia taratibu za kumwabudu Mungu kupitia uimbaji zimebadilishwa. Hata hivyo, mwimbaji huyu ameonyesha kuwa juhudi na shinikizo zao hazina mashiko kwa sababu ni wao hawasomi Bibilia, kuielewa na kuifasiri vizuri. Tazama *Kielelezo 13*.

### Kielelezo 13

Kamba	(Tafsiri)
<i>Mwitinda muyasya uthaithi ni mwalyule, Somai mbivilia na muimyalyula nesa, Satani ai mwalimu wa uthaithi ituni, Atanamba kwika nai na kwikwa kuu nthi.</i>	Mwashinda mkisema ibada imegeuzwa, Someni Bibilia na kuifasiri vizuri. Shetani alikuwa mwalimu wa sifa mbinguni Kabla kufanya dhambi na kutupwa duniani.

*Kielelezo 13* kimeangazia suala la ufahamu wa kile kinachofahamika na kisichofahamika. Mwimbaji ameshambulia mwelekeo-funge wa wazee kuhusu ufahamu wa kumwabudu Mungu. Scholar Mumo amesisitiza kwamba wazee hao hawajui jinsi ya kumwabudu Mungu kwa sababu hawasomi Bibilia na kuifasiri vyema. Hivyo, mwimbaji amekosoa mtazamo wa kijadi kuhusu ufahamu wa kumwabudu Mungu.

kulingana na mawazo ya Hutcheon (1988) amesema kuwa mtindo wa uhalisia wa kihistografia hutumiwa na watunzi ili kupinga simulizi kuu kwa kupuuza umaarufu wake. Simulizi kuu hupendelea mtazamo au mfumo fulani kuhusu uwasilishaji wa tungo za fasihi. Kwa mfano, *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) ulioimbwa na Scholar Mumo umetumiwa kukosoa mtazamo wa kimapokeo unaopendelea kukashifu wahubiri na waimbaji wa nyimbo za kisasa za injili. Mwimbaji wa wimbo huu anapendekeza mtazamo usiopendelea ujadi uzingatiwe. Suala la 'waombezi' limekithiri katika jamii ya Wakamba. Tazama *Kielelezo 14*.

### Ukosoaji wa Dhana za Upendeleo

Waimbaji wa nyimbo za kisasa za injili za Kikamba zilidhihirisha matumizi ya usohalisia wa kihistoria kukosoa dhana za upendeleo. Hii ni

### Kielelezo 14

Kamba	(Tafsiri)
<i>Mwikilya mwona mavasita maivoya, Kukemea maimu, na kuumya maveva. Kuvakwa, kuvakwa mauta, na kuvanda mbeu, Muyasya mena mayini, ni athaithi ma Satani.</i>	Kila mnapoona wachungaji wakiomba Kukemea majini, na kutoa mapepo. Kupakwa kupakwa mafuta, na kupanda mbegu Mnasema wana majini, ni waabudu wa Shetani.

*Kielelezo 14* kimerejelea baadhi ya masuala ambayo yanatiliwa shaka na wanajamii kama vile suala la 'waombezi' wenye kuombea watu na kisha kudai pesa. Suala hili limefanya wanajamii wengi watilie shaka mahubiri na maombi yanayofanywa na wahubiri wa kisasa wa sampuli hii na kudai wanatumia nguvu za majini. Wanajamii hawafahamu kwa nini wanaoombewa wapakwe mafuta, wauziwe yale mafuta na pia waambiwe wapande mbegu ili wabarikiwe. Scholar Mumo amekosoa walengwa wake wanaonenea vibaya maombi yanayofanywa ili

kutoa mapepo kwa sauti kali. Mwimbaji huyu haoni ni kwa nini watumishi wa Mungu wanapotumiwa kufanya miujiza wanasemekana wametumia nguvu za majini. Licha ya kuwakosoa wapinzani wake kwa sauti kali, Scholar Mumo katika wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) amepunguza makali yake na kukubaliana na wapinzani wake kwamba kuna mchanganyiko wa watumishi katika huduma anayoitetea. Hivyo, mwishoni mwa wimbo huu amechora usambamba wa watumishi wa Mungu na watumishi wa Shetani. Tazama kielelezo cha 17 kinachosimulia:

**Kielelezo 15**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Ve andu makwina, na angi matekwina.</i>	Kuna watu wanaimba na wengine wasioimba.
<i>Ve atavanyia na angi mateatavanyia.</i>	Kuna wahubiri, na wengine wasiowahubiri
<i>Andu ma kuvoya na angi mena ndaimoni.</i>	Watu wa kuomba na wengine wenye mapepo.
<i>Athukumi ma Ngai na athukumi ma Satani.</i>	Watumishi wa Mungu na watumishi wa shetani.

Hivyo, *Kielelezo 17* kimeonyesha kwamba mtunzi wa wimbo *Ngoma ya Yesu* (Densi ya Yesu) licha ya kukosoa simulizi za wapinzani wa nyimbo za kisasa za injili amesadiki kwamba wapo watumishi wa kweli wa Mungu na kuna watumishi wa Shetani. Kukiri kuwepo kwa uwingi wa watumishi vilevile ni kukiri kuwepo kwa miungu wengi wa kutumikiwa katika jamii

ya kisasa ya Wakamba. Hii ni kulingana na mawazo ya Hutcheo (1988) kwamba hakuna ukweli mmoja lakini kuna kweli nyingi. Mwishowe anawarai wasikilizaji wake waache kuhukumu nani ni nani lakini wamwachie Mungu jukumu la kuhukumu. Tazama *Kielelezo 18*.

**Kielelezo 16**

<b>Kamba</b>	<b>(Tafsiri)</b>
<i>Twisoma muikasilile, nikenda muikasililwe.</i>	Tunasoma msihukumu ili msihukumiwe
<i>Sila ti witu, usililo ni wa Yeova.</i>	Hukumu si yetu, hukumu ni ya Jehovah.

Mtunzi amewakumbusha kwamba Biblia inasema wasihukumu wasije wakahukumiwa kwa sababu hukumu ya haki ni ya Mungu. Aidha, amewakumbusha wasikilizaji wake maneno yaliyosemwa na Yesu katika Kitabu cha Matayo Mtakatifu (13:30) na Luka (6:37) ambayo ameyachopeka katika wimbo wake.

usohalisia wa kihistografia kukosoa dhana za upendeleo katika jamii husika. Hivyo, kipengele cha usohalisia wa kihistografia katika nyimbo za kisasa za injili za Kikamba ni muhimu katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui ya wimbo husika.

**HITIMISHO**

Utafiti huu uligundua kwamba waimbaji wa nyimbo teule za kisasa za injili zilitumia usohalisia wa kihistografia kukosoa simulizi za kihistoria zinazoshikiliwa na wajadi. Aidha, mtindo huu hutumiwa kutilia shaka uwezekano wa historia kuwa inasimulia uhalisia kamili. Kadhalika, mtindo wa usohalisia wa kihistoria ulitumiwa na watunzi wa nyimbo teule za kisasa za injili kukosoa mtazamo wa kiuongozi kwa misingi ya kijadi kama vile ukoo na mzawa wa kwanza. Vilevile, mtindo huu ulitumiwa na watunzi wa nyimbo za kisasa za injili ili kuchanganya uhalisia na fantasia katika tungo zao wakilenga kusimulia hali halisi ya jamii husika. Waimbaji wa nyimbo za kisasa za injili walitumia mtindo wa usohalisia wa kihistografia kukuza mvutano wa kimawazo baina ya kizazi cha kijadi na kizazi cha kisasa. Mwisho, mtindo wa

**MAREJELEO**

- Akuno, E. (2005). Understanding a National Culture through Music Education: The Kenyan Experience. *African Musicology Online*, 1(2), 7-21.
- Best, S. & Keller, D. (1991). *The Postmodern Theory Critical Interrogations*. London: Routledge.
- Cahoon, L. (1996). *From Modernism to Postmodernism: An Anthology Expanded*. Wiley-Blackwell.
- Chitando, E. (2000). Songs of Praise: Gospel Music in an African Context. In *Exchange* 29(4), 296-310.
- Cockrell, D. (1987). Of Gospel Hymns, Minstrel Shows, and Jubilee Singers: Towards Some

- Black South American Music. In *American Music* 5(4), 417-432.
- D'haen, Theo L. (1995). Magical Realism. In: *Spanish American Fiction*. Hispania. 38 (2): Pp 187-192.
- Gloag, K. (2012). *Cambridge Introduction to Music Post-modernity in Music*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Harvey, D. (1989). *The Condition of Post-modernity*. Massachusetts: Blackwell Publishers.
- Hicks, S. (2004). *Explaining Postmodernism: Skepticism and Socialism from Rousseau to Facault*. Arizona: Sholargy Publishing.
- Hutcheon, L. (1988). *A Poetics of Postmodernism: History, Theory, Fiction*. New York: Routledge.
- Ingalls, M. M. (2010). *Awesome in this place: Sound, space, and identity in contemporary North American evangelical worship*. University of Pennsylvania.
- Kidula, J. N. (1998). *Sing and shine': religious popular music in Kenya (television, gospel music)* (Doctoral dissertation, Dissertation, University of California, Los Angeles).
- Kimugung, S. (2015). Mitindo Mamboleo ya Ubaadausasa katika Nyimbo Teule za Jamii ya Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja. *Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret: Kenya (Haijachapishwa)*.
- King'ei, G., & Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kramer, J. (1996). *Postmodern Concepts of Musical Time*. New York: Routledge.
- Lewis, B. (2001). Postmodernism and Literature. In: *The Routledge Companion to Postmodernism*. Sim S. (Ed.), London and New York: Routledge. Pp 121-133.
- Lyotard, (1984). *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Manchester: Manchester University Press.
- Malone, B. (1984). Music, Religious of the Protestant South. In: Samuel, S. Hill (ed.). *Mercer University Press*. Pp. 529.
- Malpas, S. (2005). *The Postmodern: The New Critical Idiom*. London: Routledge.
- McHale, B. (1987). *Postmodern Fiction*. Great Britain: Mithuen & Co. Ltd.
- Muathe, H. M. (2012). *A Relevance Theoretical Analysis of the Communicative Effect in Selected Contemporary Kikamba Gospel Music* (Doctoral dissertation).
- Mugenda, O. & Mugenda, A. (2003). *Research Methods, Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: ACT
- Mwendwa, R. M. (2020). *A Lexical Pragmatic Approach to the Study of Metaphorical Expressions Used in Selected Kikamba Gospel Songs* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Nicol, B. (2009). *The Cambridge Introduction to Postmodernist Fiction*. New York: Cambridge University Press.
- Nyairo, J. (2008). Kenya Gospel Soundtracks: Crossing Boundaries, Mapping Audiences. In *Journal of African Cultural Studies*, 20(1), 71-83.
- Omojola, O. (1987). *Compositional Style and African Identity: A Study of Modern Nigerian Art and Music*. A PhD Thesis University of Leicester. Leicester: (Unpublished).
- Ritgerotil, B. (2006). *Postmodernism and The Simposons: Intertextuality, Hyperreality and Critique of Metanarratives*. London: Routledge.
- Taylor, V. & Winquist, C. (2002). *Encyclopedia of Postmodernism*. London: Routledge.



Tenna, M. (2019). Postmodernism in Selected Ethiopian Diasporic Novels in English. A *PhD Thesis, Addis Ababa University (Unpublished)*.

Wamitila, K. (2008). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishing Ltd.

Wise, S. & Stanley, L. (2002) *Breaking Out Again: Feminist Ontology and Epistemology* (2<sup>nd</sup> Edition). London & New York: Routledge.